SOMO LA 6

Ufahamu Hukupa Nuru ya ukweli wa Biblia

MAUDHUI MAKUU YA BIBLIA

Tuliona katika somo namba 5 kuwa maandiko yaweza kutuhekimisha hata tupate wokovu kwa njia ya kuwasiliana na akili ya mtu na hekima na maelezo ya fikra ya Uungu –

"…hamjalisoma neno lililonenwa na Mungu, alisema, Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo?"

Ni wazi Yesu alikuwa akiwambia watu ya kuwa ni lazima WASOME Maandiko (yaani Agano la Kale, ambayo ndiyo waliyokuwa nayo tu wakati ule) ili kujua kusudi la Mungu na mambo mengine husika.

Tunapoanza kujifunza mambo makuu yanayohusu mafundisho ya Biblia, ni jambo la kimsingi kujitahidi kwanza tupate kwa ujumla dhana ya maudhui makuu na ujumbe wake. Wengi wamefanya jambo la kuhuzunisha kwa kufungua kurasa zake wakiwa tayari na mambo waliyoshikilia hapo awali kuhusu mafundisho, na wanafikia kujaribu kuunda na kupanga mafundisho yake kulingana na mambo hayo yaliyowasakama akilini.

Tukiiendea Biblia kwa mawazo yaliyo wazi, itatufunza dhana ya Mungu na kutupa utaratibu wake.

Muhtasari wa kimsingi wa kusudi kuu la Mungu katika uumbaji wake imesemwa kwa njia rahisi lakini kwa mpigo katika maandiko:

1. Mnasaba wa utukufu na heshima kwa Mungu kutoka kwa viumbe wake vinampa raha, na hii ndio kusudi la kuumba vitu vyote. Viumbe vyafaa kumpendeza Mungu, sio Mungu kupendeza vilivyoumbwa:
   Ufunuo 4:11 "Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa."Dhana ya kumpendeza Mungu haijitokezi hapa lakini yafaa ieleweke hivyo…"for thy pleasure they are and were created"

2. Kusudi la Mungu la pili lahusu nchi ambayo hatimaye itajawa na utukufu wake:
   Hesabu 14:21 "Lakini hakika yangu, kama niishivyo, tena kama dunia hii nzima itakavyojawa na utukufu wa BWANA."

3. Namna itakavyojawa na utukufu wake ni vile itakavyojawa na maarifa ya Mungu na njia zake: (angalia kwa makini kuwa maarifa na utukufu zinabadilishana nafasi katika kueleza jinsi ulimwengu utakavyojazwa)

Isaya 11:9 “Hawatadhuru wala hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua BWANA, kama vile maji yanavyoifunika bahari.”

4. Njia ya kumheshimu na kumpa Mungu utukufu, kwa hivyo, ni kumjua na kutenda mapenzi yake kwa hiari.
   Zaburi 50:23 – “Atoaye dhabihu za kushukuru, ndiye anayenitukuza, naye autengenezaye mwenendo wake, nitamwonyesha wokovu wa Mungu.”

5. Wale wanaojua na kwa hiari yao wenyewe wanaamua kutenda mapenzi yake, kwanza kwa matarajio na hatimaye katika hali halisi ya ajabu na iliyojaa utukufu, wanakuwa sehemu ya jamii ya Mungu na wanaitwa wana wake wa kiume na wa kike na wanalivaa jina lake.
   Isaya 43:5-7 “Usiogope; maana mimi ni pamoja nawe; nitaleta wazao wako toka mashariki, nitakukusanya toka magharibi ; nitaiambia kaskazini, Toa; nayo Kusini, Usizuie; waleteni wana wangu kutoka mbali; na binti zangu kutoka miisho ya dunia. Kila mmoja aliyeitwa kwa jina langu, niliyemuumba kwa ajili ya utukufu wangu, mimi nimemwumba, naam, mimi nimemfanya.”

Hili ni kusudi la Mungu ambalo ni rahisi na wazi kutoka kwa maandiko; yaani kujaza ulimwengu huu na watu ambao watahiari hatimaye kutenda mapenzi yake na kulitukuza jina lake. Mafundisho na tafsiri zote kila mahali zafaa kupimwa kwa kulinganisha na maudhui haya ya Biblia. Kila kitu kinaegemea hapa. Hii ndio sababu kuu ya kuwepo kwetu – kwa mapenzi yetu huru kumpa Mungu utukufu na heshima. Hii ndiyo njia ya pekee ya kuwa sawa na furaha ya kweli.

Tunapoisoma Biblia kuanzia mwanzo hadi mwisho, tunaona ya kuwa ujumbe wake hautuelekezi tu kwa masuala ya jinsi gani na kwa nini lakini pia tunaona hali itakayopelekea kusudi kuu la Mungu litakavyotimizwa. Ni dhamira yetu kuwa masomo haya yatatuongoza katika safari hii katika Neno la Mungu na kuonyesha vitu hivi kwa kina ili kila mtu aweze kufahamu jinsi mambo yatakavyokuwa na vile inavyotuhusu.

Tunapoanza safari hii, tutaanza kuona ujumbe ulio thabiti ambao unadhihirika kwetu – ujumbe ambao unatangaza na kupanua zaidi mawazo yetu kuhusu haya maudhui makuu ya Mungu ya kuujaza ulimwengu na utukufu wa jina Lake kwa huduma na utiifu hiari wa wale wanaotenda mapenzi yake.

Tunaanza kuona mpango huu ukijidhihirisha katika milango ya kwanza michache ya kitabu cha Mwanzo, kitabu cha kwanza katika Biblia. Dhambi ilipoingia ulimwenguni kupitia kwa hao wawili walioumbwa mwanzo, twapata kuona kuwa mbali na hukumu ya kufa na kufukuzwa toka katika bustani ya Eden, ahadi ya matumaini ilitolewa pia:

Ahadi ya Mungu katika Bustani ya Eden:

Mwanzo 3:15 “Nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.”

Tunaelewa fika kuwa ahadi ya watu kuishi duniani milele sio jambo la kutazamia na kuchangamkia kama hapatakuwa na mabadiliko makubwa kuhusiana na uovu unaokithiri na hali mbaya inayokumbuka mazingira ya dunia hii.

Ahadi iliyo katika kifungu hiki ni ile ya ukombozi kutoka kwa NGUVU ya dhambi na mauti kupitia MBEGU ya mwanamke.

Ahadi za Mungu kwa ABRAHAMU:

Mwanzo 13: 14-15 "Bwana akamwambia Abramu, baada ya Lutu kuwa umejitenga naye, inua macho yako sasa, uangalie mahali hapa ulipo kaskazini, na kusini, na mashariki, na magharibi. Kwa maana nchi yote uionayo nitakupa wewe, na uzao wako milele. "

Kumbuka maoni ya mtume Paulo kuhusu ahadi hii:

Wagalatia 3:16 "Basi ahadi zilipewa Ibrahimu na uzao wake. Hasemi, Na kwa mbegu, kana kwamba ni nyingi; lakini kama moja, Na kwako mbegu, ambayo ni Kristo. "

Kutokana na hili ni wazi kwamba "uzao" ni Kristo; lakini angalia ni nini hiyo inamaanisha kwetu ikiwa tuko ndani ya Kristo:

Wagalatia 3: 28-29 "Hakuna Myahudi wala Myunani, hakuna mtumwa au huru, hapana mwanamume wala mwanamke; kwa maana nyinyi nyote mmekuwa kitu kimoja katika Kristo Yesu. Na ikiwa ninyi ni wa Kristo, basi nyi ni uzao wa Ibrahimu, na warithi kwa kadiri ya ahadi.

Tutagundua kuwa, masuala haya yanashughulikiwa Mungu anapoendelea kuwapa ahadi watu wake wenye haki ambao ni uzao wa mwanamke.” Kila ahadi inayoongezwa, kwa namna fulani, inachangia vipengele vingine kwa ahadi ya awali – ikionyesha maendeleo ya mahusiano ya Mwanadamu katika kusudi hili la Mungu. Angalia kwa makini yale yaliyomo katika ahadi kwa Daudi na jinsi yalivyoelezwa kwa mapana na nabii Isaya:

Ahadi za Mungu kwa Daudi:

2 Samweli 7:12-13,16 “ Nawe siku zako zitakapotimia, ukalala na baba zako, nitainua mzao wako nyuma yako, atakayetoka viunoni mwako, nami nitaufanya imara ufalme wake. Yeye ndiye atakayejenga nyumba kwa jina langu, nacho kiti cha enzi cha ufalme wake nitakifanya imara milele. Na nyumba yako na ufalme wako, vitathibitishwa milele mbele yako (yaani Daudi akiwa hai). Na kiti chako nitakitafanya imara milele.”

Angalia kwa makini ahadi hizi zinamwonyesha Daudi mambo mambo matatu:

1. Mzao wake Daudi ndiye atakayeimarisha na kuwa mtawala wa Ufalme wa Mungu milele;
2. Tukio la ahadi hii litatokea baada ya kifo cha Daudi;
3. Ya kuwa, Daudi atakuwepo mwenyewe na atashiriki katika ufalme huo; Daudi hana budi kufufuliwa kutoka kwa wafu.

Mtume Petro anasema kitu kuhusiana na ahadi hii ya “mzao” aliyeahidiwa Daudi –

Matendo 2:30 “ Basi kwa kuwa (Daudi) ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, ya kwamba katika uzao wa viuno vyake atamketisha mmoja katika kiti chake cha enzi.”

Maandiko matakatifu ni ya ajabu kweli kwani hatuachwi kukisia ni nani anayelengwa hapa. Kifungu kingine kinachofuata kikijengea juu ya maudhui haya ni:

Isaya 9:6-7 “ Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto mwanamume; na uweza wa kifalme utakuwa begani mwake; naye ataitwa jina lake Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, mfalme wa Amani. Maongeo ya enzi yake na Amani hayatakuwa na mwisho kamwe, katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa hukumu na kwa haki, tangu sasa na hata milele. Wivu wa BWANA wa majeshi ndio utakaotenda hayo.”

Kifungu hiki kutoka katika kitabu cha Isaya kinakuza zaidi ahadi hii iliyonenwa kwa Daudi; na kwa kufanya hivyo inakuwa wazi kuwa, kuongezea kwa hilo la ufalme kutokuwa na mwisho, utasimamiwa na mwana wa Mungu ambaye atamwakilisha Mungu, na ufalme huo utakuwa wa amani na haki. Maelezo kama haya yalifanywa na malaika aliyemtokea Mariamu. Ni jambo la kuvutia kuona kuwa maneno na maana ni mamoja, na maendelezo ya ujumbe wa Mungu kumhusu Kristo –

Luka 1:32-33 “ Huyo atakuwa mkuu, ataitwa Mwana wa Aliye juu, na Bwana Mungu atampa kiti cha enzi cha Daudi; baba yake. Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na ufalme wake utakuwa hauna mwisho.”

Ni muhimu kutambua kwa kuangalia katika maandishi ya injili kuwa Yesu hakuweza kutimiza ahadi hii katika kipindi chote cha maisha yake. Aghalabu katika maisha yake, Yesu akiwa na wanafunzi wake walihubiri ujumbe huu (au “injili” – “habari njema”) wa Ufalme wa Mungu. Wanafunzi wake mara nyingi walitarajia achukue hatamu za uongozi awe mfalme juu ya taifa la Israel, lakini kwa masikitiko makubwa hili halikutimia. Badala yake, akiwa na umri wa miaka 33 tu, Kristo alisulubiwa. Hata hivyo alifufuka kutoka kwa wafu baada ya siku tatu, na akawa na wanafunzi wake kwa muda kama ilivyorekodiwa katika:

Matendo 1:3 “Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai, akiwatokea muda wa siku arobaini, na huyanena mambo yaliyohusu ufalme wa Mungu.

Twaona hapo juu kuwa ingawa Kristo hakuwa amechukua hatamu za kuwa Mfalme, anaendelea kuzungumzia jambo hili. Tena, wanafunzi wakamuuliza swali kuhusiana na MAJIRA ya tukio hili. Jibu lake –

Kifungu cha 7 “ (Yesu) Akawambia, Si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba aliyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe.”

Halafu –

9-11 “Akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakasimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja JINSI IYO HIYO mlivyomwona akienda zake mbinguni.”

Tusichukulie maneno hayo muhimu hivihivi maana yana uhusiano na kusudi la Mungu katika kutimiza mapenzi yake mwishowe.

Tukio hili halijatokea, ni jambo linalosalia kutazamiwa kwa matarajio makubwa, matayarisho na kwa kukaa macho. Kurudi kwa Yesu kwa mwili na hali halisi hapa duniani ikawa ni msingi wa mafunzo ya mitume –

Matendo 3:19-21 “Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana; apate kumtuma Kristo Yesu mliyewekewa tangu zamani; ambaye ilimpasa kupokewa mbinguni HATA zije zamani za kufanywa upya vitu vyote, zilizonenwa na Mungu kwa kinywa cha manabii wake watakatifu tokea mwanzo wa ulimwengu.”

Angalia kwa makini kifungu hiki kinavyoonyesha uthabiti wa kusudi la Mungu kotekote – kutoka mwanzo (“tokea mwanzo wa ulimwengu”) – na pia kuwa haya yametabiriwa. Ni lazima tutambue pia kuwa hakuna jambo katika mpango wa Mungu linalotendwa kiholela au ovyoovyo. Mungu ana mpangilio wa “wakati mwafaka” alioteua katika kutimiza matukio yake –

Matendo 17:30-31 “Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anawaagiza watu wote wa kila mahali watubu. Kwa maana AMEWEKA SIKU atakayowahukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu Yule aliyemchagua; naye amewapa wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua katika wafu.”

Ni jambo la kimaumbile kufikiria kuwa hakuna kitakachobadilika na ya kuwa mambo yataendelea kama awali; lakini inatupasa kutambua ujumbe huu wa maandiko kuwa Mungu ana

mpangilio maalumu kwa majira yake, na mpango huu wa Mungu waendelea kupangika na utatukia kama alivyokusudia na ilivyotabiriwa.

Biblia ina vifungu vingi mno kuhusu kusudi la Mungu halisi katika kurasa zake tangu mwanzo hadi mwisho. Tia maanani kifungu hiki na onyo hili kutoka katika mlango wa mwisho wa kitabu cha mwisho cha Biblia –

Ufunuo 22:12, 20 “Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja name, kumlipa kila kila mtu kama kazi yake ilivyo. Yeye mwenye kuyashuhudia haya asema, Naam; naja upesi. Amina.”

Masomo yatakayofuatia yatachunguza kwa uketo ujumbe wa maandiko kuhusiana na nia na kusudi la Mungu.

MASWALI ya somo la 6

1. Kusudi kuu la Mungu la uumbaji ni nini?
2. Kulingana na Biblia, itatukia wapi?
3. Kusudi la Mungu litatimizwa vipi?
4. Mwanzo mlango wa tatu watueleza ya kuwa hukumu kwa wazee wawili wa mwanzo, ahadi ya matumaini pia ikaja. Walipewa adhabu gani?
5. Mwanadamu alihukumiwa kwa nini?
6. Ahadi ilikuwa gani?
7. Fafanua maana ya neon “ukombozi”.
8. Ibrahimu aliahidiwa nini?
9. Ni vitu gani vitatu vinaonyeshwa katika ahadi za Mungu kwa Daudi?
10. Ni vitu gani viwili vya ziada vinavyojitokeza katika kitabu cha Isaya kuhusiana na ahadi kwa Daudi?
11. Ahadi ya Mungu kwa Mariamu kumhusu Yesu ilikuwa nini?
12. Je, imetimizwa?
13. Malaika waliwaahidi nini wanafunzi wakati wa kupaa kwa Kristo?
14. Ujumbe wa maandiko kuhusu mwelekeo wa mpango wa Mungu ni nini?